# Kuanzisha Hatua Maalum

## Januari 2024

Skena hapa chini kusoma mtandaoni

NORTHUMBRIA POLICE & CRIME COMMISSIONER

NORTHUMBRIA POLICE

CPS

Kuripoti, au kufikiria kuhusu kuripoti ubakaji au unyanyasaji wa kijinsia kwa polisi kunaweza kuchocha sana. Pia tunaelewa kuwa wazo la kesi kwenda kortini na kulazimia kuzungumza juu ya kile kilichokupata kwenye kesi kuonekana kuwa la kuogopesha na la kiwewe. Hii ikiweza pia kujulikana kama kutua ushahidi.

Kuna usaidizi ambao unaweza kutumika ili kukusaidia kupata faraja na kujaribu kupunguza hofu na dhiki wakati wa mchakato huu. Hizi huitwa 'Hatua Maalum' – hatua za kukusaidia kutoa ushahidi. Sio lazima utumie hatua maalum ikiwa hutaki, lakini mwongozo huu utakusaidia kuchunguza chaguzi zinazopatikana na mchakato wa jinsi hatua maalum zinaweza kutumika.

## Nani ana haki ya kuchukua hatua maalum?

Mashahidi walio katika mazingira magumu na walio na hofu wanaweza kuomba hatua maalum:

- Shahidi aliye katika **mazingira magumu** ni pamoja na – watu chini ya miaka 18; watu wenye ulemavu wa kimwili au kiakili au hali ambayo itaathiri uwezo wao wa kutoa ushahidi wao mahakamani.

- Shahidi **aliyetishwa** ni pamoja na – watu ambao wamepitia aina Fulani za uhalifu ikiwa ni pamoja na:ubakaji na unyanyasaji wa kijinsia, utumwa wa kisasa na makosa yanayohusisha silaha. Mashahidi waliotishwa pia wanajumuisha watu ambao wana hofu au kufadhaika kuhusu kutoa ushahidi.

Kwa hivyo kama umepitia ukatili wa kijinsia utaweza kuuliza hutua maalum.



## Ni hatua gani maalum ninaweza kuuliza?

### Skrini

Skrini au paneli zinaweza kuwekwa karibu na mlango wa mahakama na sanduku la mashahidi. Skrini zitakutenganisha kumuona mshtakiwa na mtu yeyote kwenye ghala ya umma, kwa hivyo hawawezi kukuona na huwezi kuwaona.Watu wengine katika chumba cha mahakama wataweza kukuona kama vile hakimu, jury, mawakili na wafanyakazi wa mahakama.

### Kutoa ushahidi kwa faragha.

Unaweza kuomba chumba cha mahakama kiondowe kila mtu ambaye hahitaji kuwa hapo. Hii ina maana kwamba wananchi hawataruhusiwa kuingia mahakamani. Hii kawaida hutolewa tu katika za kipekee, zilizo nyeti sana.

### Kuondolewa kwa wigi na gauni

Majaji na mawakili wanavua wigi na gauni wakati wewe unatoa ushahidi wako. Hii kwa ujuma hutumiwa tu na watu walioainishwa kama mashahidi walio hatarini.

### Wapatanishi

Ikiwa umeorodheshwa kama shahidi aliye katika hatari, mpatanishi anaweza kukusaidia ikiwa unahitaji usaidizi ili kuelewa kikamilifu na kujibu maswali unayoulizwa.

### Misaada ya mawasiliano

Iwapo umeorodheshwa kama shahidi katika mazingira magumu, visaidizi vya mawasiliano vinaweza kukusaidida kuelewa na kujibu maswali unayoulizwa kwa kutumia visaidizi kama vile ubao wa alama au michoro.

## Ni hatua gani maalum ninaweza kuuliza?

**Kiungo cha moja kwa moja**

Hii inamaanisha kuwa unaweza kutoa ushahidi kupitia kiunga cha kuona cha moja kwa moja kutoka chumba cha faragha. Hii inaweza kuwa kutoka kwa chumba kiliko ndani ya jengo la mahakama au kwingineko (sehemu ya ushahidi wa mbali). Utaweza kuona yeyote anayeuliza wewe maswali kama vile wakili au hakimu. Hutaweza kumuona mshtakiwa lakini kila mtu katika mahakama anaweza kukuona kwenye kiungo cha televisheni. Idadi ndogo ya mahakama zina teknolojia ya hatua mbili maalum, ambayo ina maana kwamba mshtakiwa atazuiwa kukuona kwenye kiungo cha televisheni. Ikiwa hutaki mshtakiwa akuone, unaweza kuomba kutoa ushahidi mahakamani na kuomba skrini (tazama hapo juu). Tafadhali muulize afisa wa polisi anayeshughulikia kesi yako ikiwa hatua mbili maalum zitakuwa chaguo ambazo zinaweza kutumika katika eneo lako la karibu.

**Uchunguzi wa kindani uliorekodiwa mapema (pia unajulikana kama usikilazji wa Kifungo cha 28)**

Hii hatua inapatikana tu kwa kwa waliyo chini ya miaka 18, watu wenye ulemavu (kiakili au kimwili), Waathiriwa-wanusurika wa kesi za unyanyasaji wa kingono au katika utumwa wa kisasa kesi kataki Mahaka ya Taji. Chaguo halipatikani kwa Mahakama yaHakimu. Unaweza kutuma ombi ya hatua hii ili ufanyiwe uchunguzi wako tofauti iliyorekodiwa katika kikao tofauti kabla ya kesi. Hii basi litachezwa kwa jury kwenye kesi, ambayo imepangwa kwa tarehe ya baadaye, wakati huo matokeo ya kesi yataamuliwa. Hakimu, mwendesha mashtaka na mawakili wa utetezi na mshatkiwa watakuwepo katika chumba cha mahakama katika kusikilizwa kwa Kifungu cha 28. Utatoa ushahidi wako kupitia kiungo cha televisheni cha moja kwa moja kutoka chumba tofauti.

Kifungo cha 28 kinatumika kusaidia mashahidi kutoa ushahidi mapema kuliko vile wangefanya. Mahakama kwa ujumla itaitumia kila mara kwa waliyo chini ya miaka 18 na watu wenye ulemavu. Ikiwa wewe ni mhasiriwa wa makossa ya utumwa wa kingono au ya kisasa na unafikiri unahitaji kutoa ushahidi  haraka iwezekanavyo, kwa sababu ya athari ya kesi hiyo kwa afya yako  ya akili, ni chaguo unaweza kuomba.

**Kwa maelezo zaidi kuhusu hatua gani maalum zinaweza kupatikana, tafadhali**

**https://www.cps.gov.uk/rasso-guide/support-give-your-evidence-special-measures-0**

## Nini kitatokea mara tu nimeamua ni ipi kati ya hatua maalum nadhani itanisaidia?

1) Unaweza kuzungumza na Afisa Msimamizi wa kesi yako (OIC) katika hatua yoyote ya kesi uchunguzi na kuwafahamisha ni hatua gani kati ya hizo maalum unafikiri zitakusaidia kuto ushahidi mahakamani

2)Afisa wa polisi atajaza fomu ya kushauri Huduma ya Mashtaka ya Taji(CPS) kuhusu ni hatua gani maalum ngependa na kwa nini

3)CPS ndio watu ambao wataomba kibali kwa mahakama kutumia hatua maalum ulichoomba na jinsi itakusaidia

4)Jaji ataamua kama atatoa au hatatoa hatua maalum. Polisi watakujulisha hakimu ameamua nini. Haya yote yanapaswa kufanyika kabla ya kesi.

Hatua maalum hazipewi kwa kawaida – hakimu ataamua ni hatua gani maalum anazoidhinisha kabla ya kesi.

**Kwa hivyo ni muhimu sana ikiwa unaweza kueleza ni kwa nini unafikiri mojawapo ya hutua maalum zinazopatikana zinaweza kukusaidia unapotoa ushahidi na jinsi zinavyoweza kuwa na matokeo bora kwako na kuhisi kuweza kushiriki. Unaweza pia kuulizwa kwa nini unafikiri moja ya hatua maalum inaweza kukusaidia zaidi ya nyingine.**

ISVA au IDVA wako na afisa wa polisi wanaweza kukusaidia kwa hili.

### ISVA auIDVAhelp wanawezaje kusaidia kwa hatua maalum?

- ISVAs au IDVAs wanaweza kujadili hatua maalum nawe na kukusaidia kuelewa kila ambacho kinaweza kupatikana kwako
- ISVA au IDVA wako anaweza kutetea mahitaji na matakwa yako na kukusaidia kueleleza kwa nini unahisi utafaidika kwa kutoa ushahidi kwa kutumia hatua maalum.
- Ikiwa unataka wafanye hivyo, ISVA au IDVA wanaweza kuwasiliana na polisi au timu ya Usaidizi wa Mahakama ya Northumbria Mwathirika na Shahidi(NVWS) ambao wanaweza pia kutuma maombi kwa mahakama kwa ajili ya hatua maalum kwa niaba yako.

## Nini kitatokea ikiwa nitabadilisha mawazo yangu kuhusu kipimo maalum ninachofikiria itanisaidia?

Ni sawa kubadilisha mawazo yako kuhusu ni kipimo gani unadhani kitakusaidia katika kutoa ushahidi. Hili likitokea, tafadhali zungumza na Afisa Mfawidhi (OIC) wa kesi yako haraka iwezavyo ili maombi mengine yafanywe kabla ya kesi. Hii husaidia kuhakikisha kwamba mipango inaweza kufanywa kwa wakati ikiwa kuna mabadiliko yoyote kwa kile kilichotolewa . ISVA au IDVA wako wanaweza kukusaidia kujadili hili na OIC.

**Mifano ya jinsi skrini na chumba cha kiungo cha moja kwa moja kinaweza kuonekana:**







### Ziara ya kabla ya kesi

Kabla ya kesi unaweza pia kuhudhuria ziara ya kabla ya kesi. Hii ni ili uweze kuangalia na upate uzoevu na jengo la mahakama na vifaa.

Huduma ya mashaidi inaweza kupanga na kukuonyesha chumba cha mahakama na baadhi ya hatua maalum unazoweza kuomba. Kwa mfano, wanaweza kukuonyesha jinsi skrini zinavyoonekana na kukupekeka kwenye mojawapo ya vyumba vya kuunganisha moja kwa moja. Hii inaweza kukusaidia kuamua kama ungependa kuuliza hatua maalum, na kama kipi

Huduma ya ushuhuda pia itakuonyesha chumba cha mashaidi, ambalo ni eneo utasubiri kabla ya kutoa ushahidi kwa kupangwa unaweza kuingia kwenye jenog la mahakama kupitia mlango tofauti, wa kibinafsi ili usiwe na wasiwasi kuhusu kufika mahali pamoja na mshtakiwa kwa kesi.

Ikiwa ungependa kuhudhuria ziara kabla ya kesi, tafadhali zungumza na ISVA au IDVA ambaye anaweza kupanga haya kupitia Huduma ya Ushahidi wa Ushuari wa Wananchi. Ikiwa ungependa wanaweza pia kuhudhuria pamoja nawe.

## Mifano:

*Beth aliwasiliana na polisi kuripoti kwamba mpenzi wake wa zamani alikuwa amembaka .*

*Pia alikuwa mnynyasaji wa kimwili na wakuamrisha walipokuwa kwenye uhusiano. Beth alikuwa na wasiwasi sana juu ya kwenda mahakamni na kuzumza juu ya kile kilichompata na alikuwa na shaka kama angeweza kukabiliana nayo .*

*Beth aliogopa sana kukutana uso kwa uso na mpenzi wake wa zamani na watu wa familia yake ambao huenda wakakuja naye kwa vile walikuwa wakimtisha pia.*

*Beth alimweleza ISVA wake kwamba angejisikia vizuri na salama zaidi ikiwa angewza kutoa ushahidi wake mahakamani lakini kutoka nyuma ya skrini, ikimtenganisha kuona mpenzi wake wa zamani na umma ambapo familia yake inaweza kuwa.*

*Beth alishauri kwamba ingawa ingekuwa vigumu kujua kwamba walikuwa huko, angehisi kuwa na uwezo wa kuzugumza kwa uhuru zaidi na hatahisi uwoga wa kutazamwa nao. ISVA ilimsaidia Beth kueleza hili kwa afisa wa polisi ambaye alitoa taarifa hii kwa CPS. Walituma maombi kwa mahakamam wakieleza ni kwa nini Beth angenufaika kwa kutumia skrini na hilo lilikubaliwa.*

*Jenny alibakwa na mwenzake usiku katika kazini . Aliripoti hili kwa polisi na kufuatia uchunguzi, mwenzake alishtakiwa kumaanisha kwamba atalazimika kwenda mahakamani kutoa ushahidi.*

*Jenny alikuwa na matatizo ya afya ya akili katika maisha yake yote, ikiwa ni pamoja na unyogovu na wasiwasi. Jenny alihisi wasiwasi sana kuhusu kwenda nje katika maeneo ya umma yenye watu wengi, hasa maeneo ambayo hakuwahi kufika hapo awali.*

*Baada ya kuzungumza na ISVA wake kuhusu aina tofauti za hatua maalum, Jenny alihisi angeweza kutoa ushahidi kwa umbali, mbali na jengo la mahakama. Jenny alieleza hayo akisubiri kutoa ushahidi mahakamani itakkuwa na athari mbaya sana kwa afya yake ya akili.*

*Jenny alisema kwamba wakati amekuwa na wasiwasi siku za awali, alipata mshtuko wa hofu na kuhisi kama hawezi kupumua. Jenny alikuwa na wasiwasi kwamba kuwa katika jengo moja na mtu aliyembaka kungezua wasiwasi wake. Jenny alisema angepate fariji zaidi akijua atasubiri kati jingo tofauti, la kibinafsi na ISVA wake*

*Afisa msimamizi wa kesi ya Jenny alieleza hili kwa CPS nao waliuliza Jenny atoe ushahidi kupitia kiunga cha moja kwa moja kutoka kitengo cha ushahidi wa mbali. ISVA wa Jenny pia alisaidia kupanga ziara ya kabla ya kesi kwenye chumba cha ushahidi cha mbali ili Jenny aweze kujifahamisha na jingo hilo kabla ya kesi na kuhakikisha kuwa anajua zaidi kuhusu kile anachopaswa kutarajia.*

# Kuanzisha Hatua Maalum

NORTHUMBRIA POLICE & CRIME COMMISSIONER

NORTHUMBRIA POLICE

CPS